**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU -TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI

# SHULE YA SEKONDARI UMBWE

S. L. P. 718
**MOSHI**

**SIMU:** 0754 950 881
0762986976/0752445705
0654923977/0758254261
Email mungayape@gmail.com

Tarehe:…………..

Unapojibu tafadhali taja,
**Kumb. Na. USS/150/VOL.II/183**

JINA LA MWANAFUNZI....................................................................……………………………

S.L.P. ............................................ ………………………………………………………….. …..

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI UMBWE WILAYA YA MOSHI, MKOA WA KILIMANJARO MWAKA…………**

## 1. UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu na kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Umbwe, kidato cha tano (V) tahasusi (combination) ya **ECAc/CBG/HGE/HGL/PCB/HKL na EBuAC** kwa mwaka wa masomo wa ………………**,**

Unategemewa kuwa mwanafunzi mwenye NIDHAMU, JUHUDI, MAARIFA na USHIRIKIANO mkubwa na watumishi pamoja na wanafunzi wenzako kwa muda wote ukizifuata ***sheria na taratibu zote za shule***. Hayo yatakuwezesha kutimiza lengo lako, wazazi/walezi na Serikali la kukupa nafasi hii ya kupata haki ya Elimu.

Shule ni ya **bweni** kwa **wavulana**, ipo Wilaya ya Moshi Vijijini, umbali wa Km.20 kutoka Moshi mjini. Usafiri wa basi upo muda wote wa mchana kutoka kituo kikuu cha mabasi Moshi mjini, panda gari ***la Kibosho – Umbwe/Lyamungo, nauli ni Tsh. 1000/=,*** utatakiwa kuteremkia kituo kinachoitwa ***kwa Raphaeli***. (Umbali wa Km 2 kufika Shuleni). Hapo utachukua usafiri wa pikipiki (Boda boda) kwa nauli ya kati ya sh. **1000/=** (bila mzigo) au **3000**/= (pamoja na mzigo).

Muhula wa Kwanza wa masomo kwa kidato cha TANO utaanza tarehe ………… Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia **tarehe …………….**, Kabla ya saa 12 Jioni na **mwisho wa kuripoti ni tarehe……………… iliyopangwa na serikali, baada ya muda huo kupita nafasi yako atapangiwa mwanafunzi mwingine.**

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2. I SARE YA SHULE

i. Aje na Suruali mbili (2) rangi **NYEUSI** yenye turn up, chini upana USIOPUNGUA inchi 16 au atashonewa akifika shuleni kwa @ sh. 22,000/= ( aje na track suit ya rangi DARK GREEN)

ii. Mashati mawili (2) meupe ya tetron ya mikono mirefu. Atawekewa nembo akifika shuleni

iii. Aje na Tai **"NYEUSI"** yenye mistari na nembo ya shule- au atazipata shule kwa @sh. **6000/=.**

iv. Anaruhusiwa kuja na pulneck ya kuvalia ndani nyeusi/nyeupe

v. Mkanda wa suruali mweusi wa ngozi upana wa kawaida usio na marembo (Nadhifu)

vi. Viatu vyeusi, vya ngozi, vya kufunga na kamba, vyenye visigino vifupi, jozi mbili (2)

vii. Soksi rangi nyeusi za kutosha.

Viii. Aje na faili la kuwekea nyaraka zake shuleni.

ix. Aje na Sweta mbili (2) au zaidi za shule rangi **DARK BLUE**, shingo ya V (Umbwe Kuna baridi)

x. Aje na T-shirt ZA SHULE 2 DARK BLUE, zenye nembo ya shule, au atazipata shuleni kw ash. 13,000/= kila moja.

xi. Track suite **nzito** Rangi ya **DARK GREEN,** (kuna kipindi baridi ni kali)

xii. **Vifaa vya Michezo**- Bukta, Tisheti na soksi ndefu za rangi kimkondo: (ECAc- **Njano**, CBG, **Nyeusi,** HGL-**Nyekundu** - HGE-**Blue, PCB – kijani, EBuAC - Nyeupe**), na viatu vya michezo rangi yeyote.

xiii. Nguo za kushindia (Shamba dress)

   a. Suruali 2 za rangi ya **BROWN** za kushindia **anaweza** kushonewa shuleni kwa sh. 22,000/= au aje ameshona iwe na turn up na chini isipungue inchi 16.

   b. Aje na T-shirt 2 shingo ya duara za **KIJIVU** zisizo na maandishi, nzito ni nzuri zaidi

xiv. Buti za mvua Nyeusi au rangi yoyote jozi moja, koti la mvua na mwavuli ni vya muhimu sana

<u>**MUHIMU**</u> ***KILA MWANAFUNZI AJE NA BIMA YA AFYA AU AJE NA TSH.50,400/= KWA AJILI YA BIMA YA AFYANI-NHIF.***

**NB:** <u>**Unashauriwa kuandika/kuweka alama vitu vyako vyote kabla ya kufika shuleni**</u>

<u>**KUMBUKA**</u>**:** *Nguo zote na mavazi yasiyo rasmi hazitaruhusiwa wakati wote uwapo shuleni, unatakiwa kuzingatia maelekezo haya na ni* kosa kubana suruali, <u>UNATAKIWA KUWA NADHIFU</u>

### 2.2 MICHANGO YA SHULE

Mchanganuo wa malipo ya shule ni kama ifuatavyo;

| S/NO | MAELEZO YA MALIPO | KIASI |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000 |
| 2. | Nembo ya Shule | 5000 |
| 3. | Kitambulisho cha Shule | 5000 |
| 4. | Tahadhari - caution money (*Haitarudishwa*) | 5000 |
| 5. | Kangafu (generator) | 10,000 |
| | **JUMLA YA MALIPO KWA MWAKA** | **Tsh. 90,000/=** |

<u>*Kumbuka:*</u> Michango ni <u>**Tsh. 90,000**</u> **-** Lipa yote kwenye account ya shule.

<u>**Inasisitizwa:**</u> **michango yote ilipwe kabla ya mwanafunzi kufika shuleni**

Malipo haya yafanyike kwenye account ya shule yenye jina: **The headmaster Umbwe Secondary School**, **Acct. No 40301200152 NMB** kwenye tawi lolote ama wakala wa NMB. Wazazi wanaendelea na ujenzi wa ukuta, na makubaliano hayo utapewa ufikapo shuleni

<u>***Tunawasihi wazazi***</u> *kuwa Baadhi ya wanafunzi* <u>***wasio waaminifu***</u> *hutumia ada na michango ya shule kwa matumizi yao binafsi. Hivyo mzazi/mlezi/taasisi wafadhili, hakikisha unalipa hela yote Benki na mwanafunzi aje na Bank-Pay-Slip ikiwa imeandikwa jina la mwanafunzi, iwe halisi sio kivuli (photocopy), Unaweza kulipia katika tawi lolote ama wakala wa NMB aliyepo karibu nawe.* ***Hatupokei fedha taslimu 'cash' shuleni***

### 2.3 MAHITAJI MUHIMU YA MWANAFUNZI AMBAYO ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI

i. Godoro (linanapatikana Shuleni na linakodeshwa **kwa mwaka Tsh. 20,000/**)
ii. Begi imara & kufuli ya kufungia. (**usije kabisa na sanduku la chuma /bati/mbao -tranka)**
iii. Mto na foronya 2 rangi ya **BLUE na** bed cover rangi yoyote.
iv. Blanket 1 la rangi yeyote,
v. shuka 2 za rangi ya **BLUE**
vi. Vifaa vya chakula (vinapatikana kwenye duka la shule)
vii. Ndoo za **Plastic 2** za lita 10 kuogea/kufulia na kuhifadhia maji ya matumizi binafsi
viii. Chupa ya maji ya kunywa
ix. Kikombe cha kuogea cha lita moja (1lt), cha plastic *(matumizi binafsi)*
x. Vifaa vya usafi wa mwili (dawa ya meno, sabuni ya kuogea na kufulia, mswaki, kitana, mafuta ya kujipaka, rangi ya viatu, brashi, taulo nguo za ndani za kutosha Kandambili jozi moja,n.k).
xi. Karatasi za chooni (Toilet papers) kumi au zaidi kwa matumizi binafsi
xii. Saa ya mkononi ni muhimu sana. Lazima

**NB: Unashauriwa kuandika/kuweka alama ya kudumu vitu vyako vyote kabla ya kufika shuleni**

### 2.4 VIFAA VYA MAFUNZO - VITABU NA VIFAA VYA KUJIFUNZIA

Shule ina vitabu na vifaa ambavyo wanafunzi hutumia kwa kushirikiana. Mwanafunzi atakayeazimishwa kitabu/kifaa asiporudisha anapotakiwa kufanya hivyo atahesabiwa kuwa na kosa la kutorudisha mali ya shule na hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake. Kumbuka kuwa upotevu wa kitabu/kifaa chochote utafidiwa kwa kutoa/kuleta kitabu kingine/kifaa cha aina hiyo wala si fedha.

Unashauriwa kununuliwa vitabu na vifaa stahiki kwa masomo husika utakayosoma hapa shule ili kukupa nafasi zaidi ya kujisomea kwa uhuru bila kutegemea vilivyopo vya kushiriki.
Vifaa vya **lazima vya** darasani unavyotakiwa kuwa navyo shuleni ni pamoja na:-

i. Madaftari makubwa (counter books) yasiyopungua 6 na mengine madogo ya majaribio na kujisomea 12(exercise books)
ii. Jalada (File) la kuweka mitihani ni muhimu sana, uje na faili mbili moja nyaraka zako na jingine mitihani yako.
iii. Disecting kit kwa wanafunzi watakao soma Biology
iv. Kamusi ya kiingereza – Oxford **English Dictionary** kwa wanafunzi wote
v. Scientific calculator (f x 991) kwa masomo ya sayansi, Biashara, na Geography **(lazima)**
vi. Mathematical set, kalamu za wino na penseli za kutosha, ufutio, rula n.k.
vii. Lab coat nyeupe kwa wanafunzi wa sayansi wote.
viii. Stop watch kwa wanafunzi wanaosoma Physics na Chemistry.
ix. **Ream mbili za karatasi nyeupe zisizo na mistari – Dublicating paper size A4 *(aina paperline au A1)* na rim moja yenye mistari kwa wanafunzi wa ECAc,CBG,HGE,PCB,HKL na EBuAC**
*x.* Kwa wanafunzi wa HGL Ream (2) moja ya A3 (Karatasi pana) na moja yenye mistari
*xi.* Stepler machine moja (1) na staple pins kwa kwa kila mwanafunzi kwa matumizi binafsi.
*xii.* Nakala ya orodha ya vitabu imeambatanishwa
*xiii.* Begi la kubebea madaftari la kuvaa mgongoni
xiv. Graph paper kwa matumizi binafsi kwa wote ni lazima isipokuwa HKL.

### 2.5 VIFAA VYA USAFI WA SHULE:

Utatakiwa kuja na vifaa vifuatavyoo kwa ajili ya usafi wa jumla shuleni;-

A. **WANAFUNZI WOTE-** wanatakiwa kuja na Sabuni ya maji (Disinfectant ya. ***DEXi***) Lt 5, fagio za chelewa 02 wenye mpini mmoja na usio na mpini mmoja.
B. **CBG** - Squizer/pusher 1 kwa ajili ya kukaushia maji, ufagio wa hard broom 1, toilet brush na kikopo chake
C. **ECAc** – Ndoo 1 ya kudekia ya chuma/bati na dekio lake la utambi na soft broom 1
D. **HGE** –Jembe lenye mpini 1 kwa ajili ya usafi, soft broom 1, toilet brush 1 na kikopo chake
E. **HGL-** Squizer, Soft broom, Reki 1 na mpini wake.
F. **PCB** – Dustpan, Panga, hard broom 1, Ufagio wa buibui 1 (wenye mpini mrefu)
G. **HKL** - Toilet brush na kikopo chake, Hard broom 1, Slasher 1 na Squizer 1
H. **EBuAC** – Jembe na mpini wake, slasher na hard broom

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

### A: SHERIA

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa **Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978**. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. **KUJITUMA, KUJITAMBUA IBADA NA NIDHAMU** **ni misingi mikubwa ya shule yetu**, hivyo haya ni ya muhimu kuyaishi ukiwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Umbwe;

1. Unatakiwa kujifunza kwa nguvu na kwa malengo, kutimiza adhma ya kuja Umbwe
2. Heshima, utii na ushirikiano kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
3. Unashauriwa kuepuka marafiki/makundi yasiyo ya kujenga ndani na nje ya shule.
4. Kushiriki Clubs, za masomo na kijamii, michezo na kazi zote nje ya kazi za darasani
5. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni ya muhimu 6. Shule inapofunguliwa unatakiwa kuripoti kwa wakati, kwenda kinyume ni kosa.
7. Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation)
8. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
9. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule wakati wote. Kutoka bila ruhusa utaadhibiwa, na utalazimika kuchangia matofali 100 makubwa kuchangia kujenga ukuta wa shule
10. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule kwa ujumla.Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
11. Kufuata utaratibu wa kutoka, na kurudi kwa wakati, utakapokuwa na lazima ya kutoka.
12. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na kutumia muda ipasavyo na kuheshimu kengele.
13. Wanafunzi wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni na kutokufuga ndevu.
14. Kushiriki vipindi vyote vya dini na ibada

### MUHIMU:

- *Mwanafunzi hapaswi kuja na **simu** shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;*
- *Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. **Ni marufuku** mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;*
- *Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa **ruhusa** na kibali maalum toka Uongozi wa Shule.*

**B: MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1. Wizi
2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 05/kukosa vipindi bila taarifa/utoro
3. Kujihusisha na masuala ya kimapenzi ukiwa mwanafunzi-Uasherati, ushoga ubakaji
4. Kuoa/kuolewa
5. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile, bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k
6. Uvutaji wa sigara ama aina zingine zinazoshabihiana
7. Kupiga/kupigana na mwanafunzi mwenzako, ama mtu yeyote ukiwa shuleni au kuwa sehemu ya ugomvi.
8. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma, mali yako ama ya mtu mwingine
9. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
10. Kudharau Bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa na alama zingine zote za Kitaifa
11. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
12. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
13. Kutoka nje ya shule bila kibali/ kutokuwa na sare za shule
14. Kumpa mtu mimba, kuharibu mimba au kushiriki kutoa mimba
15. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
16. Kukataa adhabu kwa makusudi
17. Kuwa na makosa madogo ya kujirudia, fomu ya onyo itatolewa mara moja tu
18. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
19. **Mwanafunzi kumiliki, kukutwa au kutumia simu** ya mkononi ama vifaa vinavyohusiana na simu akiwa shuleni, na vifaa vingine vinavyotumia umeme mf. Redio, pasi nk.
    Kumbuka hatupokei wala kutunza simu za wanafunzi. **Tuna simu ya shule**

Ni wajibu wa mwanafunzi kuheshimu, kutii, na kuhakikisha anatunza maadili yetu, Imani zetu, utamaduni wetu, na ajue popote atakapokuwa akiwa mwanafunzi anabeba dhamana ya Taifa, jamii, familia na shule yetu.

**NIDHAMU NI MSINGI WA KUTIMIZA MALENGO YAKO UKIWA UMBWE SEKONDARI.**

***NB:*** ***Maamuzi ya makosa haya, hayatahitaji mzazi kujulishwa zaidi ya mara moja ili kutimiza adhabu ya kumsimamisha shule mwanafunzi, ni wajibu wa mwanafunzi kuishi na kufuata taratibu zote za shule. Mzazi/mlezi/shirika/mfadhili na mwanafunzi, soma na kuzielewa sheria za shule na kuyakubali kwa kusaini fomu ya makubaliano ya utii.***

**UTARATIBU WA VIPINDI VYA DINI UKIWA SHULENI**

**Shule yetu siyo ya kidini**, ila inaheshimu, inasisitiza na kutoa nafasi kwa **wanafunzi wote** kuabudu kwa imani zao, kwa kuzingatia na kuheshimu ratiba, sheria za shule na za nchi, maelekezo na mipaka ya imani zingine ukiwa shuleni. Hivyo basi,-

- **Ni wajibu na ni lazima mwanafunzi kuhudhuria vipindi vyote vya DINI yake awapo shuleni**
- Vipindi /Ibada zote zinafanyika **SHULENI** na si vinginevyo isipokuwa kwa ibada maalumu

**Vitabu vya dini kwa ajili ya sala na vipindi vya dini hapa shuleni ni kama ifuatavyo:**

i. **Waislamu** - Waje na Quran Tukufu
ii. **Wakatoliki** - waje na Misale ya Waumini, Biblia na Rozari Takatifu, chuo kidogo cha sala, kitabu cha mafundisho kidato cha tano (Mf. *Jimbo Katoliki Moshi*)
iii. **Waprotestant** chini ya CCT, SDA na Madhehebu mengine ya Kikristo- walete Biblia na vitabu vya nyimbo vya madhehebu husika, na machapisho mengine kulingana na imani yao.

**Fahamu** Ibada zote zinafanyikia shuleni isipokuwa kwa siku maalumu kwa kibali cha kutoka nje ya shule

**FEDHA ZA MATUMIZI MADOGO MADOGO** (*Pocket money*)

Mzazi/mlezi anaweza kumpa mwanafunzi fedha kiasi kwa ajili ya matumizi binafsi, kisiwe cha kumsumbua mtoto ama kumuingiza kwenye vishawishi. Tunashauri fedha hizi zitunzwe bank kuondoa vishawishi vya wizi. Ama kwa Mhasibu wa shule kwa

**Namba ya shule ya M-pesa 0758 437 286** *(Tafadhali epuka kutuma fedha kwa watu wasio rasmi)*

**4. VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU - Zijazwe kabla ya kufika shuleni**

a. Fomu **"A"** ya mzazi na mwanafunzi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayo tolewa na shule
b. Fomu **"B"** ya uchunguzi wa afya (Medical examination form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara atakaporipoti shuleni. -*(Hakikisha unafanyiwa vipipo sahihi)*
c. Fomu **"C"** ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
d. Fomu **"D"** ya AHADI ya mwanafunzi
e. Fomu **"E"** ya Usajili.
f. Pamoja na kukamilisha fomu zote hapo juu, mwanafunzi atatakiwa kuja na;-

i. Picha tatu (3) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.
ii. Aje na kivuli (photocopy) za **<u>cheti cha kuzaliwa</u>** na cha matokeo yake ya kidato cha nne lakini pia (Original Result slip) ambayo utarudishiwa ukishapokelewa)
iii. Picha tatu (3) za mwanafunzi alizopiga na shati la shule.

**<u>Muhimu:</u>**

Soma maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Fomu zote zilizoambatanishwa na zijazwe kwa ***ukamilifu kabla ya kuripoti***. **Fomu "E"** itajazwa utakapofika shuleni.

**<u>NB:</u>** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume fedha ama kupewa maelekezo ya kuwasiliana na usiowajua.**

**<u>TAFADHALI</u>;**

*Upatapo ujumbe wowote kuhusu mwanafunzi/mtoto wako usitume chochote, ni vema ukawasiliana na uongozi wa shule kupata ukweli wa taarifa husika.*

**UMBWE - MTI SAFI;**

**MTI SAFI HUZAA MATUNDA BORA** (kauli mbiu ya shule)

**KARIBU SANA UMBWE SEKONDARI**

…………………………………………

ELIREHEMA P. MUNGAYA

**MKUU WA SHULE**

**OFIS YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI**
**SHULE YA SEKONDARI UMBWE S.L.P 718, MOSHI.**

# FOMU A

## HATI YA MAKUBALIANO

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI UMBWE,

S. L. P 718,

**MOSHI**

**YAH. KUKUBALI NAFASI, KUFUATA SHERIA NA MASHARTI YA SHULE**

**Mim**i (mwanafunzi)………………………… ……………………………………………**..**…………
kutoka shule ya sekondari…………………………… ……….na kupata daraja (*division*)……………
Nakubali nafasi ya kidato cha **tano**, Mchepuo.........................niliyopewa katika shule hii.

Ninakubali na kuwa nitatii na kuzifuata sheria za shule na za Nchi zilizoko na zile zitakazotolewa muda wote ikiwepo ratiba ya shule, kwa mujibu wa Sheria na taratibu za uendeshaji shule.

Naahidi kuwa nitawaheshimu na kuwatii walimu, wafanyakazi wasio walimu wote wa shule na kama walezi wangu na wanafunzi wenzangu wote bila kujali tofauti zetu zozote.

Nitawatii na kushirikiana na wote watakaoteuliwa/kuchaguliwa kuwa viongozi wa serikali ya wanafunzi kwa mujibu wa sheria.

Naahidi kuwa nitakuwa mwanafunzi mwaminifu wakati wote, pia kuwa nitasoma kwa bidii zangu zote kwa manufaa yangu binafsi, familia yangu, jamii na Taifa kwa ujumla.

Naahidi kuyatunza mazingira, mali za umma, binafsi na wenzangu muda wote.
Natambua kuwa nikikiuka ahadi hizi nitapoteza nafasi yangu hapa shule.

<u>Ewe Mwenyenzi Mungu Nisaidie</u>

JINA LA MWANAFUNZI …………………………………………SAHIHI ……………………

JINA LA MZAZI//MLEZI………………………………………SAHIHI……………………

ANUANI YA MZAZI/MLEZI/MWANAFUNZI ………………………………………………

NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI/SHIRIKA (i.)…………………… (ii)…………………

Namba ya Whatsapp…………………..Barua pepe (e-mail)…………….….. ……….. Tarehe……... …..

Mtendaji/Mwenyekiti wa kijiji/mtaa - Jina……………….……….Na. ya Simu…………………

Sahihi……………………………… Tarehe………………… Muhuri

Mtendaji Kata - Jina…….…………………………..Na. ya simu…………………….

Sahihi……………… Tarehe……………. (Muhuri) ………… ………

Mwalimu aliyempokea mwanafunzi……………………… sahihi……………Tarehe........./....../2024

## THE PRIME MINISTER'S OFFICE
## REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
**MOSHI DISTRICT COUNCIL**

**UMBWE SECONDARY SCHOOL**
**P. O. BOX 718, MOSHI.**
**MOB: 0754 950 881**

**FORM B**
**MEDICAL FORM**

To be completed by medical officer from a recognized **Government Hospital/Recognized Hospital**

Full Name of Student…………………………………Sex/Male……………….

Blood count (Red and White) ……………………………………………..

Stool examinations …………………………………………………………..

Sexually Transmitted diseases………………………………………………….

T.B …………………………………………. Skin………………………….

Eye test……………………………………..Ears………………………………

Chest……………………………………….Spleen………………………………

Abdomen……………………………………………………………………….

**ADDITIONAL INFORMATION**

E.g Physical defects/impairment pediatric disorders…………………......................................
……………………………………………………………………………………...............
………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………..

I certify that the above is fit / unfit to pursue studies as stated above.
Signiture ………………………………………………………………………………

**MEDICAL OFFICER**

DATE……………………………Rubber Stamp……………………………………………

**NOTE**: Student should send or bring the completed form to school together.

**OFIS YA WAZIRI MKUU -TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI**

**SHULE YA SEKONDARI UMBWE**
**S.L.P 718, MOSHI.**

**FOMU C**
**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Andika majina kamili *(Sawa na kwenye cheti cha kuzaliwa/kuhitimu kidato cha nne)*
(i) Majina unayotumia shule …………………………………………………………………………...…
(ii) Majina ya nyumbani (kama unayo)……………………………………………… ………………….
Una cheti cha kuzaliwa (NDIYO)/ (HAPANA). Namba ya cheti cha kuzaliwa…………………….... …….

| | JINA | BABA | UKOO | UMRI | TAREHE YA KUZALIWA |
|---|---|---|---|---|---|
| **LAKO** | | | | | |
| **LA BABA** | | | | | |
| **LA MAMA** | | | | | |

**2. NYUMBANI**

Kijiji / Mtaa ……………………………………Kata..................................................................
Tarafa ……………………..Wilaya……………………….Mkoa………………………..

**3.** Anwani ya nyumbani S. L. P………………………………… SIMU……………………….

**4.** Kukiwa na tatizo taarifa ipelekwe kwa nani…………………………………………………..
Uhusiano na wewe……………………………………………………………………….
Anafanya kazi gani na wapi…………………………………………………………………
Namba yake ya simu (i)…………………………………… (ii)…………………………………..

**5.** Wazazi na ndugu:
Baba yuko hai? ............................ Mama yuko hai? ...................
Baba ana watoto wangapi? ................wavulana……………wasichana………..
Wewe ni mtoto wa ngapi? .............. Baba ana wake wangapi?................ wewe ni mtoto wa mke wa ngapi …..….mko wangapi kwa mama huyo? ...........wewe ni wa ngapi kwa mama huyo? ...............

**6.** Dini yako …………………………….….. Dhehebu……………………………………...

**UNAOWATEGEMEA**

**7.** Unaishi na nani na wapi? .............................Simu yake (i)………..…………(ii)……………...…
Nani anayekupa mahitaji ya shule (*kama sio mzazi/mlezi tajwa*)……………………………
Simu yake (i)…………..……………………… (ii)……………………………………

Toa sababu kama siyo mzazi/ Mlezi ..........................................................................................
……………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

**Jina lako……………………………Sahihi……………………Tarehe…………………….**

*<u>KUMBUKA:</u> Kutoa taarifa za uongo ni kosa la jinai. Unatakiwa kutoa taarifa sahihi.*

# OFIS YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI
## HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI

**SHULE YA SEKONDARI UMBWE**
**P.O.BOX 718, MOSHI**

## FOMU D - AHADI YA MWANAFUNZI

**(Fomu hii ijazwe na mwanafunzi, mzazi/mlezi na picha za wazazi/walezi ziambatanishwe)**

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi mwanfunzi ………………………………………….. Kidato ……………

Ninaahidi kufuata sharia, taratibu na kanuni zote za shule ikiwa ni pamoja na kutoshiriki katika migomo, fujo ama kufanya makosa kwa makusudi yakiwepo makosa ya jinai.

Ninaweka ahadi ya kuwa mwanafunzi mtiifu kwa walimu, serikali ya wanafunzi, na wote wanaowajibika nami kwa kipindi chote cha masomo niwapo shuleni Umbwe sekondari.

**SAHIHI** ………………………………………… **TAREHE……………………..**

**AHADI YA MZAZI**

Mimi mzazi wa mwanafunzi ……………………………………………. Kidato cha ………….. mwaka…………………ninakiri kukubaliana na sheria, taratibu na kanuni za uendeshaji wa shule ya sekondari Umbwe, kushiriki vikao vya wazazi, kutoa michango ya shule na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule kwa kipindi chote mwanangu atakapokuwa akisoma kwa mujibu wa sharia.

<u>Ewe Mwenyenzi Mungu Nisaidie</u>

**MAJINA YA WAZAZI/WALEZI (Wanaotambulishwa shuleni na picha zao**

1. **Jina……………………………………………..UHUSIANO........................**

   **NAMBA YA SIMU……………………………. /…………………………….**
   **Namba ya NIDA…………………………………………**

   **SAINI.......................................................... TAREHE...................................**

2. **Jina……………………………………………..UHUSIANO.............................**

   **NAMBA YA SIMU……………………………. /…………………………….**

   **Namba ya NIDA…………………………………**

   **SAINI.............................................................TAREHE.........................**

3. **Jina……………………………………………..UHUSIANO...........................**

   **NAMBA YA SIMU……………………………. /……………………………**

   **Namba ya NIDA…………………………………**

   **SAINI.............................................................. TAREHE..........................**

4. **Jina……………………………………………..UHUSIANO.............................**

   **NAMBA YA SIMU……………………………. /……………………………..**

   **Namba ya NIDA…………………………………**

   **SAINI.............................................................. TAREHE...........................**

## OFIS YA WAZIRI MKUU -TAMISEMI
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI**

**SHULE YA SEKONDARI UMBWE**
**P.O.BOX 718, MOSHI**

**FOMU E**
**FOMU YA USAJILI WA MWANAFUNZI.**

1. JINA…………………………KIDATO CHA……………TAHASUSI……………
2. Kumb. Na ya barua ya Uhamisho/Kupangiwa
3. Shule alikotoka…………………………………………………
4. Tarehe ya kuingia……………………………………
5. **Fedha za uendeshaji (Tsh. 90,000/) Amekamilisha……………………….**
   **Hajakamilisha anadaiwa Tsh. ……………………………………………………………**

**6. UKAMILISHAJI WA MAHITAJI:**

i. Sare ya shule: Amekamilisha/ Bado Anadaiwa…………………………………..
   ………………………………………......................................................................
   ……………………………………………………………………………………
ii. Vifaa vya masomo: Amekamilisha/ Bado
   Anadaiwa……………………………… ……………………………………………
   ………………………………………..
   ........................................................................................................................iii.
   Amekamilisha - Ream………………Bado………….
iv. Vifaa vya Bwenini matumizi binafsi Amekamilisha/ Bado ……………………….
   ……………………………………………………………………………………..
v. Vifaa vya usafi.

1. Dekio aina ya Pusher/squizer ( ) 2. Ufagio wa chelewa ( ) 3. Soft Broom ( )

4. Ufagio wa bui bui ( ) 5. Hard broom ( ) 6. Brash ya Chooni ( ) 7.Sabuni ya maji( )8. Jembe ( )

9. Slesha( ) 10. Ndoo ya kudekia na dekio lake la utambi ( ) 11.Reki 1 yenye mpini ( )

Amekamilisha mahitaji yote **NDIYO** ( ) **HAPANA** ( )

Yaliyobaki yatakamilishwa Tarehe…………….Jina……………….…………..Sahihi……………..

**JINA LA MHASIBU**……………………SAHIHI……………………TAREHE…………………

**JINA LA MWAL.** ………………….SAHIHI…………. TAREHE …………..

**HAKIKISHA INAJAZWA NA KUWEKWA KWENYE FAIL LA MWANAFUNZI KWA KUMBUKUMBU ZAIDI**
**UMBWE SECONDARY SCHOOL (SUGGESTED BOOKS)**

Parents/ Guardians are advised to buy the following books for their students according to his combination so as to facilitate his A-level studies.

**1. ACOUTANCY:**

i. Business Accounting by Frank Wood Vol.1, &2,12th edition
ii. Maheshwari Advanced Accouting Vol 1&2, 11th Edition
iii. Review QNs, By MUNGO 1&2
iv. Review QNs By Sir. Silunka 1&2

**2. COMMERCE**

i. Commerce its Theory and Practice by Evelyn Thomas ii. Essential of Commerce in East Africa by S. A. Buh iii. A text book of Commerce by J. C. Singha and V.N. Mugali, iv. A text book of commerce by Dinah Kamasanyu

**3. HISTORY**

i. Adu Bohein (Ed) General History of Africa Vol. VII Africa Under Domination 1880-1983.-UNESCO ii. Learning Advanced history PP II, Idrissa Msuya **muhimu** iii. Carton J.H. Hayes Conteporary Europe since 1870-1958 iv. Denis Richadr: An illustrated History of Modern Europe 1789-1974 7th Edition (1985).

v. Walter Rodney : How Europe Under developed Africa.

vi. Normal Lowen 2013 Mastering of Modern World History-**muhimu**

vii. Yasin Saleh PP 1&2 Essential History viii. Learning Advanced African History, Idrissa Msuya **muhimu** ix. A. Boahen, General History of Africa Vol VII, Africa Under Foreign Domination 1880-1935…..**Muhimu**

x. A.A Mazrui, General History of Africa, Vol VIII; Africa Since 1935 xi. Ajayi, General History of Africa, Vol VI; The Nineteeth Centuary Until 1880….**Muhimu**

xii. B. A. Ogol, General History of Africa, Vol V, Africa from 16th to 18th Centaury

**4. ENGLISH-ENGLISH LITERATURE - NOVELS.**

1. The Beautiful Ones Are Not Yet born.
2. A man of the people.
3. His Excellency the Head of the State.
4. A season of Waiting.
5. Encounter From Africa **POEM.**
1. A Wonderful Surgeon.
2. Selected Poems.

**PLAYS.**

1. Betrayal in the City.
2. I will Marry when I want
3. An Enemy of the People. **ENGLISH STRUCTURE.**

i. English Language for Advanced Level Students, By James Songore Kajare ii. Nicolaus Asheli, Paper 1&2 iii. Advanced Literature iv. An introduction to language- Masija S.J.

v. Advance level English, Practice Approach New Syllabus By Nicodemus Asheli.

vi. Grammer and Composition Hand book Glencoe Mc Growth.

vii. Speech Communication 3rd, edition By William Brooks/ Robert W Leath. viii. Communication Skills Theory And Practice By Michel Kadeghe. **5 GEOGRAPHY.**

i. General Geography by R. B. Bunnet. ii. **Review paper 1&2 2012-2021** iii. Regional Focal Studies for Advance By Msabila D. T iv. Practical Geography by Zisti Kamili or D. T Msabila v. Physical Geography By Msabila D.T.

vi. **Pamphlets of Map sheets and Photographs by Mtegetwa** vii. Geography An integrated Approach by David Waugh

**6. ECONOMICS.**

**i. ESSENTIAL FOR A-LEVEL ECONOMICS paper I&II Lazima By Ambros Odhiambo…Muhimu sana** ii. Economics Review QNs and ANs PPI&PPII, 2010-2019 iii. Micro Economic theory By M.L.Jhingan iv. A text book of Economics by Ashaq Husein.

**v. Economic for Advance level Paper I & Paper II And Professional Studies by Ambilikile. Cha muhimu**

**7. BIOLOGY:**

i. Guide to Dissection by H.G.Q. Rowert ii. New understanding Biology for Advanced Level (4th Edition) by Glenn and Suzan Toole. iii. Biology Science 3rd Edition by D. . Taylor.

iv. Review F5&F6

v. Function Approach 4th Edition by M.B.V. Robert.

vi. Understanding Biology. **vii. Biology by TIE** muhimu viii. Cell Structure and Organization. ix. Principles of Biology. x. Dissecting set.

**8. CHEMISTRY:**

i. Arun Bahl..et al Essentials of Physical Chemistry, 2014, S. Chand ii. Arun Bahl, et al..A text book of Organic Chemistry, 2015, S. Chand iii. Mark Daniel and Hermes Damian S. Physical Chemistry with General Chemistry by APE iv. E.N. Ramsden, Calculation for A'level Chem 4th Ed, 2014, Oxford v. Dr. S.K.Jain, Conceptual Chemistry for class XI, 2012, S. Chand vi. Dr. S.K.Jain, Conceptual Chemistry for class XII, 2012, S. Chand

**9. BAM:**

i. Sillem septine I (2015) "BASIC APPLIED MATHS" 1st Edition Gdy publication. F5&F6, ii. Kawia Yahya and Mosha Immaculate 2017 "BASIC APPLIED MATHEMATICS REVIEW" problems and solutions 2001 - 2016 APE network

iii. Scientific calculator

iv. Kiiza Respicius and Mwangine Lugano 2010,Basic Applied Mathematics; 1,Edition,, Nyambari Nyangwine,

**10. GENERAL STUDIES:**

i. Joannes B. and Sospeter M.D (2010); Understanding Advanced Level General Studies ii. Gervas Zombwe, General Studies for Advance level Education

iii. Zisti Kamili (2017), General Studies, A-Level iv. (ETAC), General Studies Contemporary Book For A-Level and Colleges (2nd Edition)

10. Advanced level Physics (7th Edition) By Nelkon & Parker
11. Advanced Physics (5th Edition) By Tom Duncan
12. Physics Review for Paper One and Paper

## 11. KISWAHILI:

i. NADHARIA YA LUGHA KIDATO CHA TANO NA SITA – NYAMBARI NYANGWINE (2018/2019)
ii. NADHARIA YA FASIHI KIDATO CHA TANO NA SITA – NYAMBARI NYANGWINE (2018/2019) iii.TAHAKIKI YA VITABU TEULE YA FASIHI ANDISHI – NYAMBARI

NYANGWINE (2028/2019) iv.VITABU VYA TIE –KISWAHILI 1 & 2 ,KIDATO CHA TANO NA SITA v.NADHARIA YA LUGHA NA FASIHI – CHRISTOPHER CHARUHAYA

**VITABU VYA FASIHI ANDISHI:**

A. **USHAIRI** i.KIMBUNGA – HAJI G. HAJI ii.MAPENZI BORA – SHABAN ROBERT iii.CHUNGU TAMU – THEOBARD MVUNGI iv.FUNGATE YA UHURU – MOHAMED KHATIBU
B. **RIWAYA** i.USIKU UTAKAPOKWISHA – MBUNDA MSOKILE ii. KUFIKIRIKA – SHABAN ROBERT iii.MFADHILI – HUSSEIN TUWA iv.VUTA N'KUVUTE – SHAFI A. SHAFI
C. **TAMTHILIYA** i.KWENYE UKINGO WA THIM – IBRAHIM HUSSEIN
ii. MORANI – EMMANUEL MBOGO
iii. KIVULI KINAISHI – SAID MOHAMED
iv. NGUZO MAMA – PENINA MUHANDO

## 12. PHYSICS

1. Principle of physics for Class XI By S.Chand
2. Advanced level Physics (4th Edition) 1993 By R. Muncaster
3. Advanced PhysicsMastering Physics Part 1 & Part 2 By C. Odas & M. Massey
4. Modern's abc Physics Class XII Part II By Satish K. Gupta
5. Advanced level Physics (7th Edition) By Nelkon & Parker
6. Advanced Physics (5th Edition) By Tom Duncan
7. Physics Review for Paper One and Paper
8. Advanced PhysicsMastering Physics Part 1 & Part 2 By C. Odas & M. Massey
9. Modern's abc Physics Class XII Part II By Satish K. Gupta

***** <u>vitabu vya TIE</u>.. Kwa masomo ya Mchepuo wako ni vya msingi sana vitakusaidia pamoja na baadhi ya vitabu vilivyoorodheshwa hapo juu** <u>Jitahidi kupata kitabu kimoja kwa kila somo unaporipoti.</u>**